

Uhusiano Wa Itikadi Na Mtazamo Wa Mtunzi

Murithi Joseph Jessee

Corresponding Author: Murithi Joseph Jessee

Date of Submission: 05-09-2018

Date of acceptance: 20-09-2018

IKISIRI

Wahakiki wengi wanapohakiki kazi za fasihi hufikiria kuwa mtazamo wa mtunzi na itikadi inayojitokeza katika kazi zake ni sawa ni kama kwamba itikadi huwa moja na msimamo wa mtunzi huwa mmoja na tengemano kila mara. Kinyume na hayo, makala haya yanania kuonyesha kuwa itikadi huwa tofauti na msimamo mwandishi pia huwa tofauti ila huwa kuna uhusiano maalum kati ya itikadi na msimamo wa mwandishi kuhusu maswala anayojadili katika kazi zake. Aidha, huwa kuna uhusiano wa historia na itikadi katika nyakati tofauti na hivyo mtunzi huathirika aidha akaunga mkono itikadi tawala au akaipinga. Tunalenga kutimiza haya kwa kumrejelea S. A. Mohamed aliyeandika vitabu vingi na makala mengi kwa kipindi kirefu kwa lengo la kuonyesha uhusiano uliopo baina ya itikadi na mtazamo wa mtunzi kwa kurejelea riwaya zake.

I. UTANGULIZI

Dhana ya itikadi imeshughulikiwa kwa muda mrefu kuanzia miaka ya 1790 (Wamitila, 2008). Ni dhana ambayo imeelezwa na kujadiliwa na kuhusishwa na maswala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Ikizingatiwa kwamba fasihi huzingatia maswala ya kijamii kisanana, ni kweli kusema kuwa dhana ya itikadi basi hujidhihirisha katika kazi za fasihi. Itikadi ndio humwongoza mtunzi kuhusu yale atakayowasilisha na namna atakavyowasilisha (Mohamed, 1995). Hivyo ina maana kuwa itikadi huwa kama dira ya kupimia mema na mabaya katika kazi ya fasihi. Hata hivyo, wasomi na wahakiki wengi wa kazi ya fasihi huchukulia kuwa msimamo wa mtunzi na itikadi zinazojitokeza huwa ni moja na tengemano na hivyo msimamo wa mtunzi huwa mmoja na tengemano kila mara. Katika makala haya tutajadili mikabala tofauti ya itikadi ili kuonyesha itikadi hubadilika, kisha tutaonyesha uhusiano wa itikadi na msimamo wa mtunzi hasa kwa kurejelea historia ya jamii na mtunzi ili kudhihirisha kuwa itikadi ni tofauti na msimamo wa mtunzi ila huwa kuna uhusiano maalum.

1.1 MITAZAMO MBALIMBALI KUHUSU DHANA YA ITIKADI

Miongoni mwa wasomi wa mwanzo kutumia dhana ya itikadi ni Cabanis Destute de Tracy katika mwaka wa 1796 kumaanisha mfumo wa fikra fulani. Dhana hii ni changamano na imeleta mijadala mingi kati ya wasomi tofauti. Ni dhana ambayo ni telezi kuelezea kwa sababu ya sifa yake ya kuweza kufasiriwa kwa njia mbalimbali kutegemea malengo na dhamira ya yule anayeitumia (Chuachua, 2011:8). Kwa mujibu wa makala hii, tutatumia itikadi kwa kuzingatia mikabala mitatu. Mikabala itakayotumiwa itajumuisha ule wa Karl Marx (1973) ambao unachukulia itikadi kama ung'amuzi potoshi, mkabala wa Louis Althusser (1981) unaochukulia itikadi kuwa jumla ya dhana za kitamaduni ambazo hutawala watawaliwa kupitia vyombo vya serikali na vya kiitikadi na mkabala wa Antonio Gramsci (1985) unaelezea itikadi kuwa ni mfumo wa mawazo ya tabaka tawala ambayo huendelezwa kwa ukubalifu na ukawaida.

Karl Marx (1977) katika *The Germany Ideology* anasema kwamba, itikadi ni fikra zote ambazo msingi wake ni mfumo wa uzalishaji mali na teknolojia. Hujumuisha maoni ya binadamu kuhusu anayoyasema na anayoyafikiria kwa siasa, sheria, maadili, dini la falsafa. Mawazo hayo hugeuka pindi mfumo huu unavyobadilika hivyo itikadi na jamii huendelea kubadilika. Itikadi ndio ambayo hueleza na kuhlalisha mfumo wa siasa na kiuchumi wa jamii. Aliona itikadi kama ung'amuzi potoshi yaani imani ya uongo. Anafafanua itikadi ya kidini ambayo hutumiwa na mifumo ya kibepari na ukabaila kuwafanya watu waamini viongozi humwakilisha Mungu, kila kitu kimepangwa na Mungu na kila mtu ana nafasi ambayo Mungu amemratibia. Hivyo kuwa tajiri ni mpango wa Mungu na kuwa masikini ni mpango wa Mungu.

Akieleza kuhusu jamii, Marx (1979) katika *Pre-Capitalist Social Economic Formations* anasema historia ya jamii zote ni mapambano ya matabaka mbalimbali. Anasema kuna uhusiano baina ya fasihi na uzalishaji mali kama vile mapinduzi yanapofanyika na kufaulu, mfumo wa uzalishaji mali hubadilika na taasisi zote za kitamaduni huchukua mkondo mwingine. Anasema kwamba wanadamu daima huwa katika harakati za kuifanya hali yao kuwa bora zaidi na ili mapinduzi yafanyike huwa na hatua tatu za kihistoria. Hatua hizi ni ishiritaki ambapo wanadamu waliishi kwa pamoja na kufaidi jamii. Hatua ya biashara ndogondogo

iliyoendeleza na kukuza tabaka la wafanyikazi na baadaye mfumo wa kibwanyenye na kibeberu uliotokana na dhuluma za wafanyikazi kwa malengo ya mabepari wenyewe. Mfumo huu ukaleta makabiliano ya kitabaka hivyo kuleta mapinduzi na kuendeleza mfumo wa kijamaa unaoleta usawa wa binadamu wote. Kwake Marx, itikadi ambazo huangazia mambo ya kidini na kiroho ni za kupumbaza na hali halisi ya kiuchumi ndio yapaswa kuelekeza imani na fikra zote za kijamii.

Eagleton (1976) katika *Marxism and Literary Criticism* and *Criticism and Ideology* anaonyesha kuwa itikadi ni fikra, amali na hisia ambazo mwanadamu hupitia katika jamii yake kwa kipindi maalum na huweza kupatikana tu kupitia fasihi. Kuelewa itikadi ni kuelewa historia ya yaliyopita na yale ya sasa kwa undani zaidi ambayo husababisha kuzinduka na kujikomboa. Kila kazi ya sanaa huchipuka kutokana na mtazamo maalum wa kiitikadi na jinsi anavyouona ulimwengu. Fasihi ni itikadi ambazo zimeelezwa kwa kutumia lugha na mbinu za sanaa wakati wa utunzi. Kwa sababu itikadi huwa na miundo na mipangilio maalum, inaweza kuchanganuliwa kisayansi. Kazi za kisanaa zinapoendelea kimuundo ndivyo ambavyo kuna mabadiliko ya itikadi kuonyesha njia mpya za kuangalia uhalisia wa ulimwengu na kuuchanganua kati ya mtunzi na hadhira yake. Aidha, lugha na mbinu za kisanaa ambazo mtunzi hutumia huwa zimejikita katika itikadi fulani za kijamii na katika ufasiri wake huweza kubadilisha au la kutegemea historia ya wakati wake. Kwa ujumla fasihi ni sanaa ambayo hujumlisha uhalisia wa yaliyokuwapo, yaliyopo na yaliyo na uwezekano wa kutokea.

Hii inadhihirisha kuwa daima kuna ufungamano baina ya mtunzi na itikadi, ikizingatiwa kuwa mwanadamu mwenyewe ndiye muumba wa kazi ya fasihi (Mohamed, 1995:8), basi kazi za kisanaa kuendelea kimuundo ni zao la kubadilika kwa itikadi ya mtunzi. Kwa hivyo kadri itikadi zinavyobadilika na kwa sababu itikadi ndio huelekeza matendo yote ya binadamu ulimwenguni (Rossiland, 1990) ndivyo mtazamo wa mtunzi kuhusu maswala ya kijamii utakavyobadilika kwa sababu mtazamo wa mtunzi huwa umefumbatwa katika ile itikadi yake inayojidhihirisha katika matendo yake.

Tunapomwagazia mtunzi S. A. Mohamed kazi zake nyingi kama Mbatia Mwenda (1990:119) anavyosema zinasawiri mazingira halisi ya jamii yake na msimamo wake mkali wa kiitikadi umemfanya ajirudie sana katika itikadi zake za kijamaa. Mwandishi huiathiri jamii na fasihi kutokana kule kukua kiakili na kiroho na pia huathiriwa na mazingira mfumo wa kiuchumi ukiwepo na hivyo kukubaliana na Mohamed (1995) kwamba mwanadamu anaishi maisha ya kuathiri na kuathiriwa na hivyo fasihi ni tokeo la taathira baina mwanadamu na mwanadamu mwenzake. Hivyo ni kusema kuwa itikadi ya mtunzi huathiriana na itikadi za jamii nazo itikadi za jamii huathiriana na za mtunzi kwani mtunzi ni sehemu ya jamii na maisha ya jamii humuathiri katika utunzi na hivyo itikadi zinazojitokeza katika kazi zake ni matokeo ya taathira za jamii na yeye binafsi.

Mohamed S. A. anadhihirisha mabadiliko kwa upande wa uwasilishaji wake kama vile katika *Asali Chungu* na *Kiza Katika Nuru* kuna hali za kiyakinifu zaidi kwa kuwasilisha wahusika kitabaka na wanaomkaribia binadamu wa kawaida na lugha yake ni ya kawaida. Kinyume na kazi kama vile *Dunia Yao* na *Babu Alipofufuka* zimejengeka katika misingi ya uhalisia ajabu na wahusika hawaaminiki kikweli. Mhakiki Mwenda Mbatia (katika mahojiano katika Chuo Kikuu cha Nairobi tarehe 11/10/2015) anaafikiana kuwa Mohamed S. A. amebadilisha mitindo yake ya kiutunzi kutoka mitindo ya kiyakinifu katika riwaya za awali hadi mitindo ya kinjozi katika riwaya za baadaye. Maoni yetu ni kuwa itikadi ndio huelekeza matendo yote ya binadamu na hivyo mitindo mpya inayojitokeza katika riwaya za baadaye za S. A. Mohamed ni ishara ya mabadiliko ya kiitikadi.

Louis Althusser (1981) katika *Ideology and Ideological Apparatuses* anaendeleza dhana ya itikadi na kusema kuwa ili kuendeleza utawala na udhibiti, serikali au watawala hutumia vyombo viwili muhimu. Kuna vyombo ambavyo huendeleza utawala na udhibiti moja kwa moja kama vile wakuu wa serikali, jeshi, polisi, magereza na mahakama kati ya vinginevyo ambavyo huendeleza udhibiti moja kwa moja. Vyombo hivi hutekeleza majukumu yao moja kwa moja hivi kwamba matakwa ya tabaka tawala hulindwa na kuhifadhiwa na kwa hivyo itikadi sio ung'amuzi potoshi bali huendelezwa kwa matumizi ya nguvu. Anafafanua kwamba vyombo vya kiitikadi kama kanisa, shule, vyombo vya habari, siasa, familia, sheria, vyama vya wafanyakazi, utamaduni pia hutumiwa kuendeleza itikadi ya tabaka tawala. Vyombo vya kiitikadi kama vile siasa hutumiwa kutawala kwa mfano utaifa, soko huria, ujamaa, demokrasia na kadhalika hutumiwa kuhifadhi hadhi ya tabaka tawala. Anasema kuwa dini ilitumika zaidi kabla ya mfumo wa kibepari kuendeleza itikadi na mawazo ya tabaka tawala.

Aidha, elimu ni chombo ambacho hutumiwa na mfumo wa kibepari ambapo kila mtu huwa na itikadi inayomuandaa kwa majukumu atakayotekeleza katika jamii yenye utabaka kama wanaonyanyaswa, mshirika wa unyanyasaji, mwendelezaji wa itikadi za tabaka tawala kitaaluma na kadhalika. Watawala huweza kudhibiti watawaliwa kwa nguvu au kwa ukubalifu wao na kwa hivyo itikadi huendelezwa ambapo kila mtu huwa ameandaliwa kwa wajibu wake katika jamii ya kitabaka hasa kupitia shule. Itikadi ambayo huendelezwa ni ya kuhifadhi hali kama ilivyo yaani maslahi ya watawala huendelea kudumishwa kwa matumizi ya nguvu na mamlaka au kwa kutumia vyombo vya kuendeleza itikadi. Kwa ujumla wake Althusser Louis anapinga mkabala wa Marx kwamba itikadi ni ung'amuzi potoshi kila mara na kuiendeleza dhana hii kwamba imani na mielekeo

ya wanadamu yaweza kutokana na matumizi ya nguvu na udhibiti wa serikali na vyombo vya kiitikadi vinavyodhibitiwa na tabaka tawala ili kuhifadhi na kuendeleza maslahi yao. Ni maoni yetu kuwa katika kazi za S. A. Mohamed ung'amuzi potoshi unajitokeza kama katika *Asali Chungu* wahusika kama Zuberi wanajificha katika dini huku wakitenda maovu na katika *Kiza Katika Nuru* wahusika kama Bwan Juba wanafanya maovu na kujificha katika dini na kuendeleza maovu kiasi kwamba jamii zao zinachukua muda mrefu kuzinduka na kuelewa ukweli. Aidha, matumizi ya vyombo vya kiitikadi vimetumiwa kama vile vyombo vya habari kutumiwa kueneza uongo katika *Kiza katika Nuru* na pia kuna matumizi ya nguvu kama mauaji ya Mvita aliyekuwa kiongozi wa ukombozi na kufungwa jela kwa Salma mchumba wake. Hii inadhihirisha kuwa mikabala ya Karl Marx na Althusser kuhusu itikadi inajitokeza katika riwaya za S. A. Mohamed na hivyo itikadi na dhana changamano zaidi kuliko ilivyofikiriwa hapo awali.

Antonio Gramsci (1985) anafanua dhana ya itikadi kuwa ni kuendeleza dhana ya ukubalifu na ukawaida. Anasema itikadi hupata nguvu zake kutokana na dhana ya ukubalifu kinyume na matumizi ya nguvu. Jamii huendelea kuwa na umoja na udhibiti huendelezwa kwa nguvu na mamlaka kama vile polisi na jeshi au kwa vigeu vingine kama jinsia, rangi, kabila na utamaduni. Hali hizi huchukuliwa kwamba ni za kawaida au za kimaumbile na kwa hivyo wanaonyanyaswa huenda hata wasijue wananyanyaswa. Jamii huendeleza itikadi hizi kwa mifumo ya kiutawala kama vile mfumo wa kuumeni, makabila tawala na tawaliwa. Kwa hivyo itikadi ni mawazo au fikra za kiutawala ambazo huleta uhusiano na umoja wa jamii kimahusiano. Kwa hivyo, ukubalifu na ukawaida huleta udhibiti wa tabaka tawala dhidi ya watawaliwa na ni muhali kutupilia mbali nguvu zinazochangia ukubalifu na ukawaida katika jamii. Kwa hivyo, itikadi huendelezwa na ukubalifu na jukumu la mtunzi na mhakiki ni kuhakiki nguvu hizi za udhibiti na njia ambazo nguvu za kisiasa zina mamlaka ya ukawaida na ukubalifu huu, kwa lengo la kutupilia mbali nguvu hizi, vikundi hivi, na mawazo haya ili kubadilisha ukubalifu na ukawaida uliopo.

Hivyo mambo yanayochukuliwa kama ya kawaida kwa jamii ni tokeo la itikadi za tabaka tawala zilizopenyezwa kwa vyombo vya itikadi zinazopendwa kama vile dini, shule, tamaduni na mashirika ya kijamii na kuendelezwa kwa mambo kama vile mifumo ya kuumeni, mahusiano ya kijinsia, makabila tawala na kadhalika; yanakubalika tu kama mambo ya kawaida yaani mambo yako hivyo kwani ndivyo yanavyopaswa kuwa. Maoni yetu ni kuwa Antonio Gramsci (1985) anaafikiana na Althusser Louis kuwa itikadi hutokana na ukubalifu ila anasema kuwa kinyume na Althusser aliyesema kuwa itikadi huendelezwa kwa vyombo mbalimbali, itikadi hutokana na ukawaida na ukubalifu yaani watu huzoea hali fulani kuwa namna fulani na kuchukulia kuwa hali hiyo hupaswa kuwa hivyo. Pale ambapo Karl Marx anaona itikadi ni ung'amuzi potoshi Gramsci Antonio (1985) anaona ni ukawaida na ukubalifu.

Kwa mujibu wa makala hii itikadi imetumiwa kumaanisha mfumo wa mawazo, fikra na imani inayomwongoza na kumwelekeza mtunzi katika kuwasilisha maswala mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mfumo huu wa fikra, imani na mawazo unaweza kutokana na ung'amuzi potoshi kama Karl Marx anavyosema, vyombo vya kiitikadi na vya udhibiti na ukubalifu kama Althusser anavyosema au kutokana na ukubalifu na ukawaida kama Antonio Gramsci. Chambilecho Mohamed (1995) itikadi ndio humwongoza mwandishi kutazama kila kipenu cha maisha na kukitolea hukumu katika ufanisi na upungufu wake. Itikadi ndio humuelekeza mtunzi katika kuwasilisha dhamira yake, maudhui yake, usawiri wake wa wahusika na kwa hivyo huathiri mielekeo na mitazamo yake kuhusu maswala mbalimbali anayowasilisha na namna atakayowasilisha hivyo kuathiri utunzi wa kazi yake yote kwa hivyo daima kuna ufungamano mkubwa baina ya mtazamo wa mtunzi na itikadi anayoiaridhia katika kazi yake. Kwa hivyo ni msimamo wetu kuwa kila mwandishi huathiriwa na itikadi fulani inayomwongoza katika kazi yake nzima. Itikadi hii inaweza kuwa inatokana mabadiliko ya mifumo ya kiuchumi na mazingira ya kijamii, inaweza kutokana na vyombo vya kiitikadi au ukubalifu na ukawaida. Hii ni kwa sababu itikadi ni dhana changamano na telezi na hubadilika kadri historia na mazingira yanavyobadilika katika kiwango cha mtu binafsi kama S. A. Mohamed na katika kiwango cha jamii. Jambo hili tunalijadili katika sehemu inayofuata kwa kina kuonyesha namna mazingira ya kisiasa na kijamii yanahusiana na itikadi na mtazamo wa mtunzi.

1.3 HISTORIA YA MTUNZI NA ITIKADI

Swala la historia ya mtunzi ni muhimu sana katika kujenga itikadi yake kutokana na dhana kwamba daima kuna ufungamano baina ya siasa na uchumi wa nchi na itikadi ni dhahiri kwamba naye mtunzi huishi katika jamii na huiandikia jamii. Achebe (1975) anasema kwamba mtunzi ni sehemu ya jamii na hawezi kujitenga na jamii anayoiandikia. Aidha, Njogu (1997) anasema kuwa msanii lazima aielewe jamii yake na muundo wa jamii hiyo kwani wahusika hutokana na hali halisi za maisha. Mwandishi hawezi kujitenga na hali zinazoikumba jamii aizungumziayo na fasihi huathiriwa na matukio ya kihistoria. Inavyodhirika ni kuwa itikadi nayo hufungamana na matukio ya kihistoria yanayomwathiri mtunzi na hivyo kadri historia inavyobadilika katika vipindi tofauti, nayo itikadi ya mtunzi huzidi kubadilika ili kuifaa jamii yake na kazi yake iwe faavu kwa

hadhira yake. Hivyo, mtunzi huathiriwa na hali za kiuchumi na kisiasa zinazoibua itikadi fulani katika vipindi maalumu.

Itikadi ndio nayo humuongoza mtunzi kuhusu atakayozungumzia na itikadi hiyo ya mtunzi hutokana mambo kama vile mwandishi alizaliwa wapi, lini, mazingira gani, kakulia vipi, alienda shule gani, amesoma vitabu gani, imani gani inayotawala katika mazingira yake na hali yake ya kiuchumi miongoni mwa mengine (Mohamed, 1995:8). Kwa misingi hii, ni muhimu kuelewa historia ya mtunzi na muktadha wake wa kihistoria kwani daima historia yake hufungamana na itikadi atakayoaridhia kwa kipindi fulani ili kukidhi mahitaji ya jamii yake. Ikizingatiwa kuwa fasihi inahusu hali ya taathira yaani mwanasanaa huathiriwa na kuathiriana na maisha na kwamba mwanadamu ndiye muumbaji wa kazi ya fasihi, nayo matendo yote ya binadamu ulimwenguni huelekezwa na itikadi maalumu katika vipindi tofauti. Hivyo basi kuna ufungamano mkubwa baina ya historia ya mtunzi na itikadi itakayojitokeza katika kazi yake kupitia kwa maswala atakayojadili, mbinu atakazotumia na usawiri wake wa wahusika hivyo kuathiri kazi yake yote na mitazamo yake kuhusu maswala mbalimbali katika vipindi mbalimbali vya utunzi wake.

Tukiangazia Said Ahmed Mohamed, alizaliwa mnamo mwaka wa 1947 kisiwani Unguja. Alisomea shule ya msingi ya Darajani Zanzibar mjini. Alijiunga na shule ya upili ya Gulioni ambayo kitambo ilijulikana kama King George VI. Alijiunga na Chuo cha Ualimu cha Nkruma mjini Zanzibar mwaka wa 1966. Alianza kufunza kama mwalimu wa shule ya msingi katika shule ya Kizimbani na baadaye akawa mwalimu wa shule ya sekondari ya Utaani mnamo miaka ya 1969-1974. Alifunza masomo ya Bayolojia, Hesabu, Kemia na Kiswahili. Wakati huohuo alikuwa akiandika hadithi fupi katika vituo vya BBC na *Deutsche Welle* mashirika ya Uingereza na Ujerumani mtawalia. Baadaye alijiunga na kidato cha 5-6 na alikuwa amepanga kufanya masomo ya sayansi lakini akakosa vifaa vya utekelezi na basi akaamua kusomea somo la sanaa.

Baadaye, alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo alihitimu shahada ya B.A katika isimu na fasihi katika mwaka wa 1976. Akarejea Zanzibar na akawa mwalimu mkuu wa shule za msingi na upili za Hamanani kwa miaka mitano. Baadaye alihitimu shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu hicho hicho cha Dar es Salaam ambapo alisomea isimu tekelezi. Mohamed alifunza katika Idara ya Kiswahili mle Chuoni cha Dar es Salam kwa muda mfupi na baadaye akajiunga na Chuo Kikuu cha Leipzig Ujerumani, ambapo alihitimu shahada ya uzamifu (Ph.D) mwaka wa 1985. Alirudi kwao Zanzibar ambapo aliteuliwa na Rais wa Zanzibar kuwa Mkurugenzi wa pili katika Taasisi ya Kiswahili na lugha za Kigeni (TAKILUKI).

Mohamed alihama na kuja Kenya kufundisha Kiswahili katika kitivo cha Elimu Chuo kikuu cha Moi mnamo mwaka wa 1987 ambapo alikuwa mwenyekiti wa kwanza Idara ya Kiswahili. Mnamo mwaka wa 1990 alijiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi bewa la Kikuyu. Mwandishi huyu baadaye alienda Ujapani na kujiunga na Chuo Kikuu cha Masomo ya Kigeni kule Osaka ambapo alipata Uprofesa. Mnamo 1997 alijiunga na Chuo kikuu cha Bayreuth, Ujerumani hadi hivi karibuni ambapo amestaafu na kurudi kwao Zanzibar ambapo kwa hivi sasa anafundisha.

Katika nyanja ya utunzi Mohammed alianza kutunga mashairi na hadithi fupi huku akiwa mwanafunzi wa shule za msingi. Kwa mujibu wa King'ei (1997) Mohammed amewahi kufanikiwa katika utunzi wa tanzu tofauti kama ushairi, riwaya na tamthilia, jambo ambalo ni nadra sana kutokea katika taaluma ya fasihi kwa sababu wasanii wengi hufungika katika utanzu mmoja peke yake (uk. 4). Baadhi ya kazi zake ni *Diwani za Sikate Tamaa* (1980) na *Kina Cha Maisha* (1984). Pia ameandika vitabu vya fasihi simulizi ambavyo ni: *Vito Vya Hekima, Simo, Milio na Tashbihi* (1980). Kazi zake za riwaya ni kama vile *Asali Chungu* (1977), *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Kiza katika Nuru* (1988), *Tata za Asumini* (1990), *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006), *Nyuso za Mwanamke* (2010), *Mkama Ndume* (2012) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2013) na *Kamwe Si Mbali Tena* (2014). Isitoshe mwandishi Mohammed S. A. ametunga tamthilia kama vile: *Pungwa* (1988), *Amezidi* (1995), *Kivuli Kinaishi* (1990) na *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000). Aidha kazi za Mohamed hazikukomea hapo kwani ameandika *Kunga Za Nathari ya Kiswahili, Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi* (1995). Vile vile ametunga *Mbinu na Mazoezi ya Ushairi*. Mnamo 1988, Mohamed alishinda tuzo ya mwandishi bora ambayo ni ya heshima kuu iliyotolewa na Chama Cha Waandishi cha Tanzania. Maswala muhimu ambayo yanazungumziwa katika kazi zake ni matatizo yanayokumba bara la Afrika na chanzo cha matatizo hayo miongoni. Maitaria (2014) anasema kuwa S.A Mohamed ameshughukia maswala kama ujenzi wa jamii mpya na uzalendo katika riwaya za mwanzo alizoandika mnamo miaka ya 1970 na baadaye akaanza kuzingatia nadharia za utunzi katika za baadaye za miaka ya 1990 na kuendelea na hivyo kudhihirisha maendeleo makubwa katika utanzu huu wa fasihi. Jambo hili linaungwa mkono na Wafula (2014) anayesema kuwa mnamo miaka ya 1990, nadharia zilikuwa zimeanza kushughulikiwa kwa mafanikio katika utunzi na uhakiki na kazi nyngi ziliandikwa kwa kuzingatia mielekeo ya kinadharia.

Inavyojitokeza ni kuwa Mohamed ni mtunzi aliyetunga kazi za kifasihi kwa zaidi ya miongo mitatu na ameishi kwa muda mrefu katika vipindi tofauti vya historia ya jamii yake. Mabadiliko mengi ya kijamii, kiuchumi na kisiasa yametokea katika maisha yake. Katika vipindi vya mwanzo mwandishi aliathiriwa sana na itikadi za kijamaa (Mbatiah 1990:118) na kuwasilisha kazi zake za awali kihalisia na kiyakinifu. Aidha, ikizingatiwa kwamba mwandishi ni mtu wa kawaida katika jamii yake anaonekana kuamini kuwa walioendeleza

mapinduzi hawakuzingatia maslahi ya wanyonge na hivyo anaendeleza itikadi ya mapinduzi sio ya watu tu bali ya asasi za utawala na kujenga jamii yenye usawa. Mohamed (1984) katika “Kupatana na Riwaya Zangu” anaafiki mabadiliko haya anaposema kuwa katika *Asali Chungu* na *Utengano* alifanya makosa ambayo ameyarekebisha katika Riwaya za baadaye kama *Dunia Mti Mkavu* na *Kiza Katika Nuru* kutokana na ubinadamu na uanagenzi. Hii inaashiria mabadiliko kadri anavyokua ndivyo anayopiga hatua kiutunzi jambo ambalo Mbatiah (1990) anakubaliana nalo na kusema kuwa S. A. Mohamed amepevuka sana katika matumizi ya nadharia ya Kimarx katika riwaya za baadaye kama *Kiza Katika Nuru* kuliko riwaya za awali kama *Asali Chungu*.

Inavyodhihirika ni kuwa kadri S.A Mohamed anavyopevuka kiusomi na kutembelea nchi tofauti ndivyo mawazo yake na itikadi zake zinaathirika kama vile matumizi ya mitindo ya uhalisia ajabu katika riwaya kama *Dunia Yao* (2006) na kuangazia maswala ya jamii pana kama teknolojia mpya kama matumizi ya tarakilishi na mitandao miongoni mwa maswala mengine yanayoiathiri dunia nzima kama inayojitokeza katika *Mhanga Nafsi Yangu* (2013) ambapo kwa mfano baadhi ya wahusika kama Yakrobich ni Wajerumani. Hii inaonyesha kuwa Mohamed S. A. ameathiriwa na kuiathiri jamii yake na hivyo itikadi yake haiwezi kuwa moja na tengamano katika vipindi tofauti vya utunzi wake. Hii ni kwa sababu itikadi ya mtunzi hubadilika ili kufungamana na mawazo yanayotawala katika kipindi fulani cha kihistoria katika jamii yake na kazi zake ziwe faavu kwa jamii yake kwani yeye ni kama mwalimu anayeifunza jamii yake. Hivyo ni kusema kuwa historia ya mtunzi ikibadilika, kama inavyodhihirika katika maisha ya S. A. Mohamed, itikadi yake hubadilika na ikiwa itikadi ndio humuelekeza mtunzi kuchagua atakayowasilishia jamii na atakayoacha, ni dhahiri kwamba mitazamo yake kuhusu maswala mbalimbali hubadilika katika mapito ya wakati hivyo mtazamo wa mtunzi sio mmoja na tengamano. Hubadilika kadri historia yake inavyobadilikana hivyo itikadi na msimamo wa mtunzi na dhana tofauti ila zinahusiana.

1.4 HISTORIA YA SIASA NA UCHUMI WA ZANZIBAR

Swala la historia ya siasa na uchumi ni muhimu kwani daima kuna ufungamano wa itikadi na hali halisi ya kisiasa na kiuchumi kwa kipindi fulani kwa sababu itikadi hufungamana na siasa na uchumi (Chuachua, 2011:24). Hii ina maana kuwa, pindi mifumo ya kisiasa na kiuchumi inavyobadilika katika vipindi maalumu nayo itikadi hubadilikana hivyo kuathiri kwa kiwango kikubwa uandishi wa mtunzi. Ni katika muktadha huu ambapo tutajadili swala la historia na uchumi wa Zanzibar ambapo tunaamini swala la itikadi linaweza kujadiliwa vyema na kudhihirika kwa uwazi.

Kwa mujibu wa Njogu (1997) katika *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani* makazi ya mwanzo yalitokana na uhamiaji wa makundi kutoka bara katika nyakati tofauti na yakawa na umoja wa kisiasa ambao ungeyafanya yaweze kukabiliana na taifa lolote la kigeni ambalo lingetishia kuvuruga umoja huo. Kufikia 500 kabla ya Kristo wageni wengi kama Waajemi na Waarabu walikuwa wakifanya biashara na mataifa ya Kiafrika yaliyokuwa yakiishi mwambao wa Afrika Mashariki. Kufikia karne ya kumi na moja, kundi la Waajemi lilikuja na utamaduni wao kukubaliwa na wenyeji wa Pemba na Unguja na hivyo walifungamana sana kiutamaduni na Waafrika. Jambo hili liliathiri utamaduni, lugha na siasa za visiwani. Kiuchumi miji visiwani ilikuwa na kuimarika sana kutokana na biashara kati ya wageni hawa na wenyeji wabantu waliokuwa wakizungumza lugha ya Kiswahili. Lugha hii iliimarika zaidi kutokana na maingiliano haya ambapo maneno ya lugha nyinginezo kama Kiarabu, Kihindi, Kiajemi kati ya nyinginezo yaliingizwa kweye lugha ya Kiswahili. Wageni hawa walichagua kulowela huko baada ya shughuli zao za kibiashara na hivyo kuifanya Zanzibar kuwa kitovu na kivutio kikubwa cha biashara na hivyo kwa sababu ya umaarufu huo mataifa ya Ulaya yalivutiwa sana. Mbatiah (2016) anasema kuwa Wareno walivamia Zanzibar katika katika karne ya kumi na tano na wakachukua hatamu za uongozi mnamo 1503 Baada ya Kristo na kutawaliwa na Kapteni Ruy Lourenco Ravasco Marques. Wareno walitawala kwa muda mrefu hadi miaka ya 1648 ya Kristo ambapo utawala wa Kisultan wa Oman ulikita mizizi na kuchukua hatamu za uongozi wa visiwa hivi vikiwa vimeimarika kiuchumi, kitamaduni na hata wakiwa na lugha walioizungumza ya Kiswahili ilioenea sana kutokana na biashara na maingiliano na wageni hawa walioamua kulowela huko na kukufanya kwao kabisa.

Ukoloni wa Kiarabu visiwani Zanzibar ulikuja pamoja na mfumko wa viwanda katika nchi za Ulaya. Malighafi nyingi ilihitajika na watumwa walinunuliwa kutoka visiwani na kusafirishwa hadi Ulaya na Bara Hindi ili kufanya kazi viwandani. Zanzibar ilikaribiana na Mwambao wa Afrika Mashariki; ilikuwa na bandari nzuri na mikarafuu ilikuwa vyema jambo lililofanya kituo kikubwa cha kibiashara na kivutio kwa wengi na salama. Mnamo mwaka wa 1741 familia ya Mazrui ilifanya mkataba na utawala wa Oman. Mohammed Uthman Al-Mazrui alikataa kuukubali utawala wa Busaidi. Jambo hili lilisababisha Busaidi kujiimarisha Zanzibar ili kuifanya kituo cha kibiashara na vile vile kituo cha kiutawala (Njogu, 1997:21).

Mnamo 1804 Seyyid Said alichukua hatamu za uongozi baada ya kumuua binamu wa babake Bader Bein Seif. Ili kuimarisha utawala wake alifanya Zanzibar kuwa mji mkuu na akahamia huko pamoja na wafuasi wake mnamo mwaka wa 1832 na hali iliyofanya Waomani wengi kuhamia Zanzibar. Chini ya utawala wa Seyyid Said, Zanzibar ilikuwa kwa haraka kama kituo cha kibiashara kati ya Waarabu na nchi ya Marekani na

Ulaya. Aidha, alianzisha ukulima wa mikarafuu ambayo ilikuwa na soko katika nchi nyingi za na hivyo wafanyakazi katika mashamba makubwa walihitajika ili kuendeleza kilimo cha mikarafuu ambayo ilikuwa na faida kubwa Tatizo ni kwamba mashamba makubwa yalipewa Waarabu waliopata wafanyakazi kwa nguvu kutoka visiwani na bara. Waafrika wenyeji wakanyimwa ardhi yenye rutuba na wakawa watwana na watumwa. Kwa upande wao, Waarabu waliendelea kujilimbikizia mali nyingi na kuwa matajiri wakubwa huku Waafrika wengi wakawa wakata na makabwela hohehahe. Kutokana na haya, Wahindi wengi walihamia Zanzibar na kuanza kufanya biashara ya kusafirisha karafuu kutoka visiwani hadi Bara Hindi.

Mnamo mwaka wa 1884-1885, kongamano la Berlin liliandaliwa na kuigawa Afrika ili kuendeleza utawala wa kibepari. Waingereza walijikita visiwani ambapo mkataba ulifanywa mnamo Julai 1, 1890 na Zanzibar iliwekwa chini ya Himaya yao. Ukoloni uliimarisha muundo wa kitabaka uliokuwepo na kuendeleza hata zaidi. Sultan wa Zanzibar alitia mkataba Aprili 5, 1897 ambao uliwapa watumwa haki na uhuru wa kupeleka mahakamani maombi ya kupewa uhuru. Watumwa hawa walipewa visehemu vidogo vya shamba na iliwalazimu wakodishe na kufanya kazi kwa mamwinyi hao. Wale ambao hawakuweza jambo hili walibakia makabwela wa ulimwengu katika ardhi yao wenyewe.

Waingereza waliwapa Waarabu nafasi kubwa lakini pale biashara ya karafuu ilipoathiriwa Wahindi walianza kuchukua mashamba ya mamwinyi walioshindwa kulipa mikopo waliokuwa wamekopa. Hali hii ilisababisha kuibuka kwa makundi manne kutokana na mivutano na mikinzano hii. Makundi hayo yaliyoibuka ni ya Waingereza na Wahindi waliofanya kazi kwenye viwanda na biashara, Waarabu waliomiliki mashamba, Waafrika wakawa wafanyakazi. Hii ilimaanisha kuwa rangi ykazia mtu ilimwelekeza katika tabaka fulani.

Hivyo jamii ya visiwani ikawa ya miundo ya kitabaka hasa kutegemea rangi ya mtu. Nafasi za kiuchumi zikanasibishwa na sura ya kimaumbile. Nafasi za elimu na kazi za juu zilizotolewa kwa Waarabu, Wahindi na Waingereza nao Waafrika walifanya kazi za nguvu. Akifafanua historia ya Zanzibar, Mukobwa (1985) anasema kuwa kufikia mwisho na karne ya kumi na tisa Zanzibar ilikuwa imekaliwa na masetla wa Kiarabu ambao walimiliki uchumi na siasa za Zanzibar. Waafrika waliachwa wakiwa maskini kwani njia za kiuchumi zilimilikiwa na Waarabu na Wazungu. Wahindi walipokuja pia waliendelea kujiendeleza kiuchumi na walijiriwa katika kazi nzuri na Waafrika walidharauliwa sana.

Mnamo 1890, serikali ya Uingereza iliweka mkataba na Sultan wa Zanzibar na kuifanya Zanzibar iwe chini ya Himaya yake. Hata baada ya mkataba huu, Waarabu na Wahindi waliendelea kupewa kazi kubwa na vyeo, huku Waafrika wakibaguliwa. Mnamo miezi ya Januari (1961), Juni (1961) na Julai (1963) Chama Cha Afro-Shirazi Party (ASP) kilikuwa kikishinda uchaguzi wa kidemokrasia kwa sababu kilikuwa na Waafrika wengi na jambo hili lingemaanisha uwezo wa kiuchumi wa mabepari wa Uingereza na Kiarabu kupunguzwa.

Vyama ambavyo vilikubaliwa kuunda serikali ni *Zanzibar and Pemba Peoples Party* ambacho kilijiunga na *Zanzibar National Party* (ZNP) na kuunda muungano na kuwa na viti kumi na vinane dhidi ya *Afro-Shiraz Party* (ASP) ambacho kilikuwa na viti kumi na vitatu (Njogu, 1997). Uhuru huu haukufurahiwa na Waafrika wengi ambapo Mohammed Shemte aliunda serikali. Nafasi za utawala na za kiuchumi zilitwaliwa na kupewa Waarabu ambao walikuwa waaminifu kwa Sultan. Mapinduzi yakawa ni ya lazima ili Waafrika waweze kujikomboa na yalitokea mnamo January 12, 1964 kwa sababu Waafrika waliokuwa wengi walinyimwa nafasi ya kuendeleza mfumo wa kiuchumi ambao ungewafaa. Hussein Ebrahim katika utangulizi wa *Tamthilia ya Mashetani* (1971) anasema kuwa mapinduzi ya Zanzibar yalibadilisha maisha ya watu binafsi na jamii za watu. Serikali ya Sultan wa Zanzibar ilipopinduliwa na *Afro-Shirazi Party* kuchukua mamlaka, mashamba makubwa yalitaifishwa na kufanywa mali ya umma. Watu wengi waliopoteza mali yao walitorokea miji ya pwani ya Afrika Mashariki kama Dar es Salaam na Mombasa. Kwa sababu wengi wao walikuwa na elimu walipewa vyeo katika serikali ya Tanganyika ambapo waliendeleza ukoloni baada ya kurithi vyeo na mienendo ilioachwa na wakoloni. Kile kisichotarajiwa kilifanywa kuwa kaida na kaida zikasailiwa na kupinduliwa.

Waliokuwa matajiri baada ya mapinduzi walikuwa masikini na wakaanza kupanda kiuchumi baada ya mapinduzi haya. Ni kama kuna kinyume mbele yaani mambo kubadilika walio juu wakawa wanaelekea chini na walio chini wakawa wanaelekea juu kiuchumi. Mapinduzi haya yaliongozwa na John Okelo (Lofchie, 1965) ambapo aliunda serikali iliyowapa mamlaka viongozi wa Chama Cha UMMA na wale wa ASP (Afro-Shirazi Party).

Baada ya muungano wa Zanzibar na Tanganyika mnamo mwezi wa Aprili 1964 viongozi wenye siasa kali kama vile Okelo waliondolewa serikalini ili kuweza kurahisisha utawala. Kwa upande wa Tanganyika, serikali ya Nyerere ilikuwa ikifanya juhudi za kuvunja taasisi za kibepari kwa kupendekeza mfumo wa ujamaa. Majukumu ya kisiasa na kiuchumi yalitekelezwa na itikadi ya ujamaa na kujitegemea. Mfumo huu ulipata changamoto nyingi kama vile kutoungwa mkono na mataifa ya kimagharibi na kutoshirikishwa kwa wananchi ipasavyo. Aidha, badala ya mali kuwa ya umma, viongozi walimiliki mali kwa manufaa yao na kuendelea kutumia vyeo vyao kwa kujitajirisha. Wale viongozi ambao walikuwa wakishikilia nyadhifa za uongozi hapo mwanzoni walitorokea nchi zingine au Tanzania bara. Wale ambao walipata vyeo hivi waliendelea kujilimbikizia mali. Kwa sababu hii kukatoka mivutano baina ya waliokuwa navyo na wasiokuwa navyo. Wale walioroka wakaendelea kuanguka kiuchumi na kuporomoka kimaisha.

Mapinduzi yaliyodhamiria kuleta usawa hayakufanikiwa jambo ambalo linajenga msingi wa wasanii wengi visiwani Zanzibar akiwemo S. A. Mohamed ambaye anajadili mivutano ya kiuchumi na kisiasa kihalisia na uhalisia wa kijamaa katika kazi zake za awali hasa *Asali Chungu*, *Dunia Mti Mkavu* na *Kiza Katika Nuru* kati ya nyinginezo. Ameonyesha vile uhuru ule Waafrika waliopata ni wa bendera tu huku wakiendelea kutawaliwa kisiasa na kiuchumi. Kwa ujumla ameonyesha ili kujikomboa ni muhimu kuchemsha ubongo kwa kutafakari na kufikiri ili kuweza kupata uhuru wa kweli kama vile Mvita anavyofanya katika *Kiza Katika Nuru*. Wakoloni pamoja na mifumo yote ya kiukoloni (ya kisiasa au kiuchumi) lazima ing'olewe.

Hata hivyo katika kazi zake za awali *Asali Chungu* na *Utengano* hajaweza kukuza misingi na nadharia thabiti za kimapinduzi, jambo ambalo anaonekana kuliimarisha zaidi katika *Dunia Mti Mkavu* na *Kiza Katika Nuru* kuashiria mabadiliko ya itikadi zake za utunzi na hivyo mtazamo wake kubadilika na kuonekana kuupinga mtazamo wake wa awali kwamba mapinduzi yanaweza kutokea ghafla na sio lazima yawe yamejengeka katika msingi maalum na nadharia thabiti. Katika *Asali Chungu* kwa mfano hamna maandalizi yoyote ya mapinduzi wala ujenzi wa urazini kati ya wanamapinduzi ni kama ni jambo la sadfa tu au bahati na kama anavyokiri katika makala ya "Kupatana na Riwaya Zangu" (Mohamed, 1984:50) aliimarika zaidi katika *Dunia Mti Mkavu* na *Kiza Katika Nuru* ambapo mapinduzi yanaandaliwa vyema na urazini kujengwa vyema kati ya wanamapinduzi.

1.4 UHUSIANO WA ITIKADI NA MTAZAMO WA MTUNZI

Mohamed (1995) anasema kuwa itikadi ni mawazo ya jumla yanayomwongoza mtunzi kutazama kila kipenu cha maisha na kutoa uamuzi kuhusu kufanikiwa au kutofanikiwa kwake. Ni kweli kuwa kila mtunzi huathiriwa na itikadi fulani katika kipindi fulani inayokuwa kama dira ya kwake kupimia mwendo wa maisha na kujibu maswali ya jamii. Itikadi hiyo ya mtunzi huweza kufungamana na itikadi za jamii yake kwani mwanasanaa huishi katika jamii maalum. Kuna itikadi za kijamii kama vile itikadi za kihalisia, itikadi za uhalisia wa kijamaa, itikadi za kibepari, itikadi za mifumo ya kuumeni na kadhalika ambazo ni mawazo ya kijumla yanayoiongoza jamii kuafikia malengo yake. Itikadi za jamii zinaweza kutumiwa kuwaunganisha watu wa mataifa au makabila mbalimbali, kuongoza sera za nchi na utekelezaji wa ujenzi wa taifa nzima. Mofolou Jean (1974) anasema kuna aina nne za itikadi za kijamii ambazo ni zile za kudumisha hali kama ilivyo, itikadi za kimapinduzi, itikadi za kiroho na itikadi za kiutopia. Itikadi ambayo jamii hufuata huelekeza imani zao, matendo yao, siasa zao, sera zao, uchumi wao, na mawazo yao kuhusu ulimwengu na namna ya kukabiliana na changamoto zinazowakabili.

Akifafanua dhana ya itikadi, Mohamed (1995:8) anasema kuwa itikadi ya mtunzi hutegemea mambo kama mtunzi alizaliwa wapi, alikulia katika mazingira ya aina gani, ana imani ipi ya kidini na nafasi ya kiuchumi kati ya mengineyo. Anasema kuwa mwanadamu ndiye anayeiumba na kuiwasilisha kazi ya fasihi na ndiye anayeathiri na kuathiriwa na maisha na hivyo kuathiriana na wenzake. Hii inaonyesha kuwa mtunzi kama sehemu ya jamii yake huathirika sana na itikadi ambazo jamii yake inazingatia katika utunzi wake na hana budi kuzingatia itikadi za jamii yake katika utunzi wake ili kazi zake ziwe faavu kwa jamii lengwa. Hata hivyo yeye kama mwalimu wa jamii yake (wa Thiong'o, 1975), huwa na jukumu la kuielimisha na hata anaweza kwenda kinyume na itikadi za za jamii kama vile itikadi za kudumisha hali ilivyo na akaendeleza itikadi za kimapinduzi kama njia ya kuifunza na kuielimisha jamii yake.

Hii ina maana kuwa, mazingira ya mwanadamu yanapobadilika basi, itikadi zake huathiriwa na huenda zikabadilika. Itikadi ndio inayotumiwa na mtunzi kupimia yale atakayowasilisha na namna atakavyowasilisha katika kazi yake ya fasihi, basi mtazamo wake lazima ubadilike na huenda hata akapinga mtazamo wake wa awali kuhusu maswala fulani na kuyatazama upya, kuyawasilisha upya na hata kuyahakiki upya. Ikiwa jambo hili litawezekana ni dhahiri basi kuwa mtazamo wa mtunzi hauwezi ukawa mmoja na ulioshikamana kwani hufumbatwa katika itikadi zinazobadilika. Kwa hivyo kadri itikadi zinavyobadilika ndivyo msimamo na mtazamo wa mtunzi hubadilika na hivyo msimamo wa mtunzi na itikadi huwa tofauti sio kitu kimoja.

Njogu (1997) anaunga kauli hii mkono na kusema kuwa mtunzi huchagua atakalowasilisha kwa jamii yake kufungamana na msingi wa itikadi yake. Hivyo ni kwamba itikadi ndio humpambanulia mema na mabaya, na yale yanayoisaidia jamii na yale ambayo ni potovu. Inavyodhihirika ni kwamba itikadi ndio huufumbata ule mtazamo wa mtunzi kuhusu maswala ya jamii hasa yale anayotaka kuyawasilisha. Tukichukulia kwamba maana za maneno na dhana ni telezi (Derrida, 1976:106) itikadi ni dhana inayobadilika kila uchao, itakuwa ni dhahiri kwamba nao msimamo wa mtunzi kuhusu maswala mbalimbali ya kijamii hauna budi kubadilika kwani itikadi ndio huongoza mtazamo wa mtunzi na kama Rossiland (1990) anavyosema itikadi huelekeza matendo ya wanadamu wote. Hivyo ni kusema kuwa hata utunzi wa mwandishi huelekezwa na itikadi na hauna budi kubadilika kufungamana na mabadiliko ya itikadi.

Itikadi nayo hutegemea mambo kama vile mtunzi kazaliwa na nani, kasomea wapi, imani yake ya dini na ngazi yake kiuchumi kati ya mengineo na kadri mambo haya yanavyobadilika ndivyo itikadi yake huathiriwa na kubadilika na mtazamo wake kuhusu maswala fulani ya kijamii kubadilika. Tukichukulia kwamba mwanadamu ndiye muumba wa kazi ya fasihi, na fasihi inahusu binadamu na mazingira yake (Njogu, 2001: ix) basi mtunzi huyaathiri maisha na kuathiriwa nayo na pia kuathiriwa na wanadamu wenzake. Hivyo ni kusema

kuwa, kadri maisha yanavyobadilika na kuathiri nyanja tofauti za maisha kama vile siasa, dini, utamaduni, elimu, uchumi na kadhalika ambayo ni baadhi ya mambo muhimu ambayo hujenga itikadi ya mtunzi, ndivyo ambavyo itikadi ya mtunzi huathiriwa na kubadilika kwa sababu itikadi ndio ambayo huelekeza ule mtazamo wa mtunzi. Basi mtazamo wa mtunzi kuhusu mbalimbali hauna budi kubadilika.

Kutokana na haya ni dhahiri kuwa daima kuna ufungamano baina ya itikadi ya mtunzi na msimamo wake kwani ndio huelekeza kazi yake yote ya kifasihi na namna atakavyowasilisha kwa jamii yake. Itikadi inapobadilika basi msimamo wa mtunzi unabadilika na hivyo yale atakavyowasilisha na namna atakavyoyawasilisha yatabadilika ili kazi zake ziwe faavu kwa jamii lengwa. Pia hufanya hivi kutimiza majukumu yake kama mwalimu wa jamii yake na ulimwengu kwa jumla, Chambilecho Achebe (1975) kwamba mtunzi ni mtu wa kawaida na sharti aitumikie jamii yake bila kujitenga nayo. Jambo hili pia linaungwa mkono na Wa Thiong'o (1975) anayesema kuwa mtunzi wa Kiafrika ni kama mwalimu wa jamii lazima awaelimishe kuhusu historia yao na hali yao ya sasa ili kuwazindua na kuwafahamisha hali zao halisi.

4.6 HITIMISHO

Katika makala hii tulidhamiria kuonyesha uhusiano uliopo baina ya itikadi na msimamo wa mtunzi kwa kurejelea S. A. Mohamed. Tumeleza mikabala mbalimbali ya dhana ya itikadi ambapo tumebaini mikabala mitatu muhimu kwa mujibu wa makala haya. Mikabala iliyojadiliwa ni ile ya Karl Marx iliyobaini kuwa itikadi ni ung'amuzi potoshi na kuungwa mkono na wahakiki wengi kama Njogu na Rossiland kati ya wengineo. Mikabala mwingine uliojadiliwa ni ule wa Louis Althusser aliyesema kuwa itikadi ni dhana inayoweza kutokana na matumizi ya nguvu ya Serikali, jeshi, magereza na vile vile vyombo vya kiitikadi kama kanisa, elimu, vyombo vya habari kati ya vinginevyo. Mikabala wa tatu uliojadiliwa ni mikabala ulioendelezwa na Antonio Gramsci anayesema kwamba itikadi ni dhana ambayo huendelezwa kwa ukubalifu na ukawaida. Kauli iliyojitokeza ni kwamba itikadi ni dhana telezi na changamano kuelezea kama wanaudunguzi wanavyosema kuwa maana ni telezi na haishikiki.

Aidha, tumeangazia historia ya Zanzibar na historia ya mtunzi ili kuona muktadha ulioibusha kazi zilizoandikwa na mtunzi huyu hasa kazi zinazorejelewa katika makala hii. Tumeweza kuonyesha kwamba, kutokana na utawala dhalimu ulioendelezwa na viongozi, kufuatia kukwama kwa njia nyinginezo zozote za kujikomboa, Waafrika waliachiwa njia ya mapinduzi pekee ili kujinasua katika utawala dhalimu. Mazingira haya ndio yaliyozua itikadi za kihalisia na uhalisia wa kijamaa zinazoonekana kujitokeza katika riwaya za awali za S. A. Mohamed. Imebainika kuwa kadri historia ilivyobadilika ndivyo itikadi ilivyobadilika, nao msimamo wa mtunzi ukazidi kubadilika kwani misimamo huelekezwa na itikadi. Kwa hivyo itikadi ina ufungamano mkubwa na msimamo wa mtunzi hivi kwamba ikibadilika nao msimamo wake huathirika na kubadilika. Hii ina maana kuwa itikadi na msimamo wa mwandishi huwa tofauti lakini kazi yake ya fasihi hubadilika kwani ndiye anayeiumba na hivyo msimamo wa mtunzi hauwezi kuwa mmoja na tengemano kila wakati hubadilika kufungamana na mabadiliko ya itikadi.

MAREJELEO

- [1]. Althusser, Louis . "Ideology and Ideological State Apparatuses" Lenin and Other essays. translated by B. Brewster, New left Books ,1981.
- [2]. Chuachua, Richard. Itikadi Katika Riwaya za Shaaban Robert. TATAKI, 2011.
- [3]. Derrida, Jacques. Of Grammatology and Writing and Difference, translated by G. C. Spivak. B John Hopkins, 1976.
- [4]. Gramsci, Antonio. Selections From Cultural Writing,. translated by D. Forgas and G. Nowel-Smith. Lawrence and Wishart, 1985.
- [5]. Hegel, George. Phenomenology of Spirit, translated by A.V Miller, Oxford University Press 1977.
- [6]. Maitaria Joseph. Mwongozo wa Kidagaa Kimemwozea. Longhorn publishers, 2014
- [7]. Marx, Karl. and Freidrich Engels. On literature and Art. International General 1973
- [8]. Marx, Karl and Freidrich Engels. The German Ideology. Lawrence and Wishar, 1977.
- [9]. Mbatia, Mwenda "Commitment in the Swahili Novel: An Appraisal of the Works of Said Ahmed Mohammed. Kiswahili, Vol. 60, 1997.
- [10]. - - Riwaya ya Kiswahili Chimbuko na Maendeleo Yake. JFK, 2016.
- [11]. Mohamed Said. Asali Chungu. Shungwaya, 1978.
- - - Kamwe Si Mbali Tena. Oxford University Press, 2014.
- [12]. - - - Kiza Katika Nuru. Oxford University Press, 1986.
- [13]. - - - Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi. E.A E. P, 1995.
- [14]. Ngara, Emmuel. Art and Ideology in African Novel: A Study of the Influence of Marxism on African Writing. Heinemann, 1985.
- [15]. Njogu, Kimani. Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar. U. O. N. Press, 1997
- [16]. Njogu, Kimani. and Rocha Chimerah .Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu. JFK, 1999.

- [17]. Osore, Miriam. "Defamiliarization in the Novels of Euphrase Kezilahabi and S. A. Mohamed"
- [18]. PhD theses unpublished, Kenyatta University, 2008.
- [19]. Rosslund, Fanon. *Marxism and Ideology*. Clarendon Press, 1990.
- [20]. Wafula, Richard. "Nadharia za Uhakiki Kama Mchakato wa Kutaalamisha Usomaji wa Fasihi" *Journal of Linguistics and Language in Education, University of Dar es Salaam* Volume 8,no.1, 2014, pp 52-69..
- [21]. Wamitila, Kyalo. *Kanzi ya Fasihi*. Vide-Muwa, 2008.

Kuhusu Mwandishi wa Makala; *Murithi Joseph Jesse*

Bwana Murithi ni mwalimu wa Kiswahili katika Chuo kikuu cha Kenyatta Bewa la Embu . Ni mwalimu mwenye tajriba pana katika ufundishaji wa lugha na fasihi ya Kiswahili. Alianza kazi ya ualimu kwenye shule ya upili ya Bute Kaunti ya Wajir mnamo mwaka wa 1998 hadi mwaka wa 2002. Mnamo mwaka wa 2003 alihamishwa hadi shule ya kitaifa ya wasichana ya limuru ambapo alipandishwa cheo na kuwa mkuu wa idara ya kiswahii mwaka wa 2008 ambapo aliendelea kufunza hadi Disemba 2010. Mnamo mwaka wa 2011 mwezi wa Januari alijiunga na Chuo kikuu cha Presbyterian huko Kikuyu. Baadaye, mnamo Septemba mwaka wa 2014 alianza kufunza fasihi ya Kiswahili katika Chuo kikuu cha Kenyatta Bewa la Embu ambapo anafunza lugha na fasihi ya Kiswahili hadi sasa. Bwana Murithi alisomea katika shule ya msingi ya Kiangungi huko Embu na shule ya sekondari ya Rukuriri huko Embu. Alifuzu vyema katika mtihani wake wa kidato cha nne na akajiunga na Chuo kikuu cha Kenyatta kusomea shahada ya elimu. Alifuzu mwaka wa 1997 masomo ya Kiswahili na dini.Mnamo mwaka wa 2000 alijiunga na Chuo kikuu cha Kenyatta tena na akahitimu mnamo mwaka wa 2002 na shahada ya uzamili katika somo la Kiswahili. Kwa sasa mwalimu Murithi amefuzu mtihani wake wa mwisho wa shahada ya uzamifu katika Chuo kikuu cha Kenyatta na anasubiri kutawazwa katika mahafala ijayo mwakani.

Murithi Joseph Jesse .” Uhusiano Wa Itikadi Na Mtazamo Wa Mtunzi.” *IOSR Journal Of Humanities And Social Science (IOSR-JHSS)*. vol. 23 no. 09, 2018, pp.75-83